# Uchumi na BIASHARA

11 TANZANIA INAVYOZIDI KUFUNGUKA KUPITIA ZIWA TANGANYIKA

12 UTALII TANZANIA NI MUHIMU KWA UCHUMI



# Wafugaji kuku wanavyolia na madalali, wataka kuku auzwe kwa kilo

Uk 13

Scanned with CamScanner

# Wafugaji kuku wanavyolia na madalali, kuku auzwe kwa kilo

Na Lucy Ngowi

KUKU ni kitoweo rahisi kwa watu wengi mijini na vijijini kutokana na ukweli kuwa kila kiungo alichonacho kinaliwa.

Mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam, Rehema Futaha, anaeleza jinsi miguu, vipapatio, utumbo pamoja na vichwa vya kuku vinavyomrahisishia kazi ya kuwaandalia watoto wake mlo.

Anasema anapotoka kwenye majukumu yake ya kila siku mara nyingi hupita kwenye maeneo ambayo viungo hivyo vya kuku vinakuwa vikikaangwa kwa ajili ya kuuzwa ambapo bei yake huanzia Sh 100 hadi 1,000 kutegemea kipande mnunuaji anachokihitaji.

"Mara nyingi katika maeneo yetu haya ya Uswahilini, miguu wa kuku mmoja huuzwa Sh 200, kichwa Sh 200, kipapatio Sh 300, maini na firigisi huanzia Sh 500 hadi Sh 1,000, paja Sh 2,500 na kidari Sh 2,500.

"Unapokuta umechoka kupika, ukanunua vipande hivyo ambavyo huwa vimekaangwa inarahisisha kuvitunga na nyanya haraka kwa ajili ya mboga ya ugali ama wali na vinaweza kuliwa bila hata kuungwa," anasema.

Rehema ni mfano wa watu wengi jijini Dar es Salaam ambao hutumia vipande mbalimbali vya kuku wa kisasa (broiler) kwa ajili ya urahisi wa kupata mboga.

Wakati kwa Rehema anasema mboga hiyo humrahisishia kuandaa mlo kwa ajili ya familia, ufugaji kuku pia ni biashara ambayo huwaongezea kipato wafugaji na wafanyabiashara wanaokaanga vipande vya kuku na kuuza mitaani pamoja na wakaanga chipsi. Sasa hivi wameingia pia madalali wanaonufaika na biashara ya kuku.

Hata hivyo, wafugaji wa kuku wa kisasa wamekuwa pia wakikumbana na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na gharama kubwa za vyakula pamoja na dawa huku kuku hao wakiwauza kwa bei ndogo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo soko hilo kuingiliwa na madalali.

Wakati wafugaji wa kuku wakilalamikia soko, wauzaji wa vipande vya kuku hususani katika jiji la Dar es Salaam na wakaanga chipsi kwao imekuwa neema kwani wamekuwa wakipata faida kubwa kuliko wale wanaowafuga kuanzia vifaranga hadi kuwa tayari kwa matumizi.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Umoja wa Wafugaji Kuku wa Nyama (broiler) jijini Dar es Salaam na Pwani, Gloria Michael, anasema waliunzisha umoja wao ambao upo chini ya Tanzania Broilers Farmers Association (Tabrofa) ili kupambana na changamoto zinazowakabili kwa pamoja.

Anasema hata hivi karibuni walikutana ili kujadili changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo hususani kushuka kwa bei ya kuku shambani.



Wafugaji wa kuku wanaona kuku wakiuzwa kwa kilo inaweza kuwa suluhisho la changamoto ya soko wanalopitia.

Anasema bei ya kuku inashuka kwa kuwa hawana sehemu sahihi ya kupeleka kuku wao kutokana na uwepo wa madalali ambao wanawapangia bei.

"Bei ya kuku hawa mwaka jana ilikuwa Sh 6,000 shambani lakini baada ya madalali kuingilia hii biashara wameshusha ikawa kati ya Sh 4,500 hadi 5,000. Wafugaji wakubwa nao wanaharibu soko la wafugaji wadogo wadogo," anasema.

Mfugaji wa kuku wa kisasa kutoka Yombo, Dar es Salaam, Ruth Kivuyo anasema madalali wanawaumiza sana kwani anapokwenda kwa mfugaji anataka auziwe kuku kwa Sh 4,500 hadi 5,000, baada ya hapo dalali huyo akienda sokoni anamuuza kwa Sh 6,500, kama ni hotelini anauza kwa Sh 8000 hadi 12,000.

"Hata kwa wale wanaofanya biashara ya kukaanga kuku kipande kimoja kwa bei ya chini kabisa kinauzwa Sh 2,500 na kuku anatoa vipande vinne. Lakini hapo bado kuna kuwa na vichwa, miguu na firigisi. Kwa muuzaji huyo kuku mmoja anamuingizia zaidi ya Sh 10,000," anasema.

Anaongeza kuwa mara nyingi mfugaji anapata faida kidogo au anajikuta msingi ukikata.

Naye katibu wa kikundi hicho, Doreen Temu, anasema wamekuwa wakikumbana na changamoto pia kwenye bei ya vifaranga na chakula cha kuku kwani vitu hivyo viko juu sana.

Anasema kutokana na vitu hivyo viwili, bila kupiga dawa huku wakiminywa na madalali, ufugaji wa kuku umekuwa wa kimazoea zaidi kwani hawapati faida.

Anaeleza changamoto nyingine kuwa ni pale dalali anapolazimisha kuingia kwenye banda ili kuona hali ya kuku na kuwaachia kuku magonjwa.

Mtaalamu wa mifugo, David Msenga anasema kifaranga kimoja kinanunuliwa kwa Sh 2,000 mpaka hatua ya kumlisha, kumpa chanjo na kuwa tayari kumuuza, mfugaji huwa amekhatumia wastani wa Sh 5,000 kwa kuku. Lakini anapokwenda sokoni, anakuta soko linamlazimisha kuuza kuku kwa Sh 5,200 mpaka 5,500 hivyo hapati faida.

Anashauri kwamba sasa ni wakati mwafaka kwa nyama kuuzwa kwa kilo, hali ambayo anaamini ingewasaidia sana wafugaji badala ya kuku kupimwa kwa kushikwa paja.

"Tunaomba serikali itoe ushirikiano katika kuainisha hizo bei angalau wafugaji wangeiona faida. Tunashauri kuku wauzwe kwa kilo angalau kwa Sh 6,000 kwa kilo kama bei ya kuanzia kwa sababu bei huwa zinabadilika badilika," anasema.

Ruth yeye anaomba serikali iweke machinjio ya kuku na hao madalali wawe wakinunua kwa kilo.

"Hii ingependeza sana kama Bodi ya Nyama itaamua kulitangazia suala hilo," anasema.

Kwa upande wake, Katimu Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Imani Sichalwe, anasema hajawahi kusikia changamoto hizo na hivyo anashauri wafugaji hao kufika ofisini kwake kwa mazungumzo zaidi.

Kuhusu suala la kuku kuuzwa kwa kilo, Sichwale anasema Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Sekta ya mifugo, Elisante Ole Gabriel, aliagiza suala hilo lifanyiwe kazi na kwamba wanajiandaa kuanza mchakato.



Wafugaji wanawalalamika kwamba muuza chipsi anapata faida maradufu ya ile anayopata mfugaji wa kuku.

# Wakurugenzi wazuiwa kupanga tozo mazao ya uvuvi

Na Mwandishi Maalumu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wakurugenzi wa halmashauri zenye masoko ya samaki ya kimataifa kuache kupanga tozo za mazao ya uvuvi bila kuwasiliana na wizara.

Alitoa msimamo huo alipotembelea mnada wa mifugo katika Kijiji cha Buzirayombo, Kata ya Bukome na Soko la Samaki la Kimataifa lililopo Kijiji cha Kasenda katika Kata ya Muganza, Chato mkoani Geita.

Waziri Ndaki pia alikagua ujenzi wa machinjio ya kisasa yanayojengwa katika eneo la mnada wa mifugo katika Kijiji cha Buzirayombo Kata ya Bukome, wilayani Chato.

Alisema wizara haitaki kusikia kero kwa wafanyabiashara kuhusu tozo zisizo rafiki katika masoko hayo likiwemo Soko la Samaki la Kimataifa la Kata ya Kirumba lililopo Ilemela jijini Mwanza.

"Kuhusu tozo niseme tu kwa wakurugenzi walio na masoko haya ya kimataifa kwa maana ya Soko la Kirumba na Kasenda, wizara hatutaki kusikia kelele katika haya masoko mnapopanga tozo zenu hakikisheni kwa masoko haya mawili tuwasiliane ili tupange tozo za kwenu na za kwetu ambazo zitakuwa rafiki," alisema Ndaki.

Mbunge wa Jimbo la Chato Dk Medard Kalemani, aliomba Serikali kupitia kwa Waziri Ndaki, kuona namna ya kuwasaidia wavuvi kwa kuwapa mikopo yenye riba nafuu na kuwanunulia nyavu ili waache kujihusisha na uvuvi usiozingatia taratibu, kanuni na sheria za nchi.

Baadhi ya wavuvi na wananchi wanaofanya shughuli za kibiashara katika Soko la Samaki la Kimataifa lililopo katika Kijiji cha Kasenda, walisema wanashirikiana na serikali kuhakikisha wanadhibiti uvuvi haramu.

Aidha, walipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa namna inavyofanya jitihada za kuboresha mazingira ya wavuvi ili sekta hiyo iwe na tija kiuchumi kwa wadau na taifa kwa jumla.



The Guardian Pg. 7 05/01/2021

# As drought looms in Longido, herders urged to sell cattle in good time

**By Guardian Correspondent, Arusha**

LONGIDO District Commissioner, Frank Mwaisumbe has advised herders in the district to better sell their livestock during this period while they are still healthy before they are being hit by the severe impacts of drought.

According to Mwaisumbe, due to low vuli rains this year, most of the district has been hit by drought thus affecting water and feeds of the animals.

"It is better for the farmers to take decision now before the animals become skinny or die due to lack of enough food, we have witnessed difficult situation for livestock keepers here due to drought brought by insufficient vuli rains, to avoid more effects, let us them sell the animals while they are healthy," the DC advised the herders.

In an interview with this paper, Mwaisumbe said that animals like cattle, sheep and goats need enough feed to survive and stay healthy, so contrary to that the animals may die.

"There are some herders who have already taken their animals to the areas with enough water and feeds, but those who are yet to do so, I advise them to sell the animals now, the livestock can be sold to the meat processing factory located at Namanga border area," he added.

He also urged the pastoralists who will sell the animals to make proper use of the monies by purchasing calves and goats once the masika rain season begins so as to sustain their business.

The official also warned some herders who have been moving their animals from Longido to Emboseri area in Kenya and West Kilimanjaro to avoid selling the animals in the neighboring country without obtaining permit from the government because doing so is against the country's laws.

"There are some pastoralists who take advantage of the drought situation to sell the animals in the neighboring Kenya to avoid tax and levies, this is not allowed and once we catch them, stern measures will be taken," he said.

Steven Kiruswa, Longindo legislator said that he has started to mobilize resources, encourage pastoralists to form groups and sell the livestock at a fair price.

"Majority of the pastoralists have been falling into the wrong hands of agents when it comes to selling their animals, this is why they are campaigning and educating them to avoid these dealers but rather form groups to sell the animals in a profitable way," he said.

He said that selling the animals will also improve their income and food security in their households.

"We are organizing a mega conference which will bring all pastoralists in Longido to discuss among other things commercial and sustainable livestock keeping, during the conference, a number of challenges facing the group will be addressed including how to fight the impacts brought by drought," Kiruswa said.

Scanned with CamScanner

# ...bn/- for expansion

sufficient to warrant business expansion.

Currently, the bank, which the Catholic Church is the majority shareholders, boosts a market capitalisation of 16.08bn/-. Its shares are hardly trades on the exchange.

It has a healthy balance sheet of 220bn/- while customer deposits amounted to 180bn/- at the end of November last year.

Prof Chijoriga said the bank aimed at providing quality financial services to all sectors of the economy in a sustainable and responsible manner in society to meet customer expectations.

MCKB operates in eight regions with 11 branches - four branches are in Dar es Salaam and one each in Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Njombe, Mwanza, Kagera and Dodoma regions.

The bank wants to expand business and reach out to more customers, especially in rural areas.

# Fish market value increases by 17pc

By DAILY NEWS Reporter

THE value of fish sold in registered markets rose by 16.8 per cent to 84.8bn/- in the quarter ending September last year from 72.6bn/- of the corresponding quarter in 2019 on account of the measures taken by the government to control illegal fishing.

According to the Bank of Tanzania (BoT)'s consolidated zonal economic performance report the increase in the value was recorded in all zones except Dar es Salaam and Central, partly underpinned by an improvement in the quantity of fish sold in the markets by 8.6 per cent to 19,784.3 [illegible]

Meanwhile, a decline in the value of fish sold in Central and Dar es Salaam zones was due to a decrease in fish imports and local catches.

To reap maximum benefits from fishing, the government recently announced plans to strengthen a crackdown on illegal fishing with stern legal measures taken against the culprits.

Deputy Minister for Livestock and Fisheries Pauline Gekul said previous anti-illegal fishing activities forced the government to spend about 1.2bn/- on crackdowns, something that should not be repeated.

She said the government had put in place plans to purchase four new fishing vessels in the India Ocean to boost fishing activities and address illegal fishing in the country.

The vessels, according to the deputy minister, will help create 45,000 employment opportunities for Tanzanians.

Councils were directed to set aside 15 per cent of their revenues accrued from livestock and fishing sector for supporting development projects in their areas, including providing loans to fishermen.

According to the CCM 2020-2025 manifesto, the government focuses on improving ports and purchasing modern fishing vessels to improve the economy through fishing activities.

The ruling party's manifesto states that major fisheries development will be on course once the fishing environment is improved to attract both small and big investors to engage in the business.

The government aims at building a big fishing port along the Coast that will attract big fishing vessels for deep sea vessels to dock.

It also looks forward to providing fishing education to local fishermen, especially on the use of proper equipment and best fishing methods.

"The purchase of new five vessels will go along with the establishment of new fish processing industries and strengthening of existing ones.

This will help create a reliable market for fish products and boost the sector," reads part of the document.

# Zim to unlock insurance against extreme weather risk

Harare, Monday

GERMANY'S state development bank KfW and the World Food Programme (WFP) have committed to contribute $2 million each, to African Risk Capacity Insurance Company Limited (ARC) to support premium financing of insurance against risks caused by extreme weather events in Zimbabwe, Treasury has said.

Zimbabwe will contribute $500,000 and this will unlock maximum insurance cover of $20 million. The ARC provides capacity building on preparedness for climatic shocks, as well as insurance against risks such as droughts.

Following the government's participation in the ARC drought risk insurance policy, complemented by the United Nations WFP Replica Policy for the 2019/20 agricultural season, Zimbabwe received a total pay-out of $1,75 million in June last year.

The pay-out assisted a substantial number of the country's vulnerable households in selected districts, through the disbursement of unconditional cash transfers to food insecure and labour-constrained households (chronically ill, older person headed households) in the worst drought-affected wards.

According to the Treasury, 77 767 households are from Chivi, Binga, Bulilima, Buhera and Uzumba.

"Zimbabwe is committed t[o] participating in the 2020/21 AR[C] programme," said the Treasury.

"To relieve fiscal challeng[es] that member states face in payi[ng] their premiums compounded by t[he] effects of the Covid-19 pandem[ic] ARC has facilitated applicat[ion] of premium subsidy from KfW [and] German Government towards [pre]mium funding for the 2020/21 [ag]ricultural season.

"KfW of German and World Food Programme (W[FP]) have committed to premiu[m] ...

Scanned with CamScanner

# Tozo za masoko ya samaki ya kimataifa kuwasilishwa wizarani

**Na Edward Kondela, Geita**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki amewataka wakurugenzi wa halmashauri zenye masoko ya samaki ya kimataifa kuacha kupanga tozo za mazao ya uvuvi bila kuwasiliana na wizara hiyo ili kuondoa kero za tozo zinazowakumba wananchi wanaofanya biashara katika maeneo hayo.

Akizungumza jana mara baada ya kutembelea mnada wa mifugo uliyopo Kijiji cha Buzirayombo Kata ya Bukome na soko la samaki la kimataifa lililopo Kijiji cha Kasenda Kata ya Muganza,Wilaya ya Chato Mkoani Geita, Waziri Ndaki alisema wizara haitaki kusikia kero za wafanyabiashara kuhusu tozo zisizo rafiki katika masoko hayo likiwemo soko la samaki la kimataifa la Kata ya Kirumba lililopo Wilaya ya Ilemela jijini Mwanza.

"Kuhusiana na tozo niseme tu kwa wakurugenzi walio na masoko haya ya kimataifa kwa maana ya soko la Kirumba na Kasenda, sisi wizara hatutaki kusikia kelele katika haya masoko mnapopanga tozo zenu hakikisheni kwa masoko haya mawili tuwasiliane ili tupange tozo za kwenu na kwetu ambazo zitakuwa rafiki." alisema Ndaki.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Chato, Dkt. Medard Kalemani amemuomba Waziri Ndaki kupitia vikundi vya wavuvi vilivyosajiliwa, wizara ione namna ya kuwasaidia wavuvi mikopo yenye riba nafuu pamoja na kuwanunulia nyavu ili kuacha kujihusha na uvuvi usiofuata utaratibu.

Nao baadhi ya wavuvi na wananchi wanaofanya shughuli za kibiashara katika soko la samaki la kimataifa lililopo Kijiji cha Kasenda wamesema wanashirikiana na serikali kuhakikisha wanadhibiti uvuvi haramu.

Aidha,wameipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi namna inavyofanya jitihada za kuhakikisha inaboresha mazingira ya wavuvi ili sekta ya uvuvi iweze kuwa na tija kwa wadau wa sekta hiyo na hatimaye waweze kunufaika kiuchumi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amekagua pia ujenzi wa machinjio ya kisasa yanayojengwa katika eneo la mnada wa mifugo Kijiji cha Buzirayombo Kata ya Bukome, Wilaya ya Chato Mkoani Geita.

Scanned with CamScanner

# Serikali inavyoendelea kuboresha sekta za mifugo na uvuvi



SOKO LA SAMAKI



WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa pili kushoto), Mbunge wa Chato, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani ( kulia) na viongozi wengine, wakikagua soko la samaki la kimataifa katika Kijiji cha Kasenda, Wilaya ya Chato, mkoani Geita. *(Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).*

# *Waziri Mashimba atoa onyo kwa wakurugenzi wa halmashauri

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wakurugenzi wa halmashauri zenye masoko ya samaki ya kimataifa, kuacha kupanga tozo za mazao ya uvuvi bila kuwasiliana na wizara hiyo.

Amesema lengo la kufanya hivyo ni kuondoa kero za tozo zinazowakumba wananchi wanaofanya biashara katika maeneo hayo.

Mashimba, aliyasema hayo juzi, baada ya kutembelea mnada wa mifugo uliopo Kijiji cha Buzirayombo, Kata ya Bukome na Soko la Samaki la Kimataifa, lililopo Kijiji cha Kasenda, Kata ya Muganza, Wilaya ya Chato, Mkoani Geita.

Waziri Ndaki, alisema wizara haitaki kusikia kero za wafanyabiashara kuhusu tozo zisizo rafiki katika masoko hayo, likiwemo Soko la Samaki la Kimataifa la Kata ya Kirumba, lililopo Wilaya ya Ilemela, jijini Mwanza.

"Kuhusiana na tozo, niseme tu kwa wakurugenzi walio na masoko haya ya kimataifa, kwa maana ya soko la Kirumba na Kasenda, wizara hatutaki kusikia kelele. Mnapopanga tozo zenu, hakikisheni kwa masoko haya mawili, tunawasiliana ili tupange tozo za kwenu na kwetu, ambazo zitakuwa rafiki," alisema.

> **Kuhusiana na tozo, niseme tu kwa wakurugenzi walio na masoko haya ya kimataifa, kwa maana ya soko la Kirumba na Kasenda, wizara hatutaki kusikia kelele. Mnapopanga tozo zenu, hakikisheni kwa masoko haya mawili...**
>
> Mashimba Ndaki

Mbunge wa Jimbo la Chato, Dk. Medard Kalemani, alimuomba Waziri Ndaki, kupitia vikundi vya wavuvi vilivyosajiliwa, wizara ione namna ya kuwasaidia mikopo yenye riba nafuu na kuwanunulia nyavu ili kuacha kujihusisha na uvuvi usiofuata utaratibu.

Baadhi ya wavuvi na wananchi wanaofanya shughuli za kibiashara katika soko la samaki la kimataifa lililopo Kijiji cha Kasenda, walisema wanashirikiana na serikali kuhakikisha wanadhibiti uvuvi haramu.

Aidha, waliipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa namna inavyofanya jitihada za kuhakikisha inaboresha mazingira ya wavuvi ili sekta hiyo iweze kuwa na tija kwa wadau na hatimaye waweze kunufaika kiuchumi.

Waziri Ndaki, pia alikagua ujenzi wa machinjio ya kisasa, yanayojengwa katika eneo la mnada wa mifugo, ulioko Kijiji cha Buzirayombo, Kata ya Bukome, Wilaya ya Chato, mkoani Geita.

Uhuru uk. 2
5/01/2021

Scanned with CamScanner